HakiElimu
Brief Na.06.2K

# Mchakato wa Bajeti Tanzania Uko Wazi Kiasi Gani?

## Matokeo kutoka kwenye Utafiti wa Kimataifa

Hii ni muhutasari wa matokeo ya uchunguzi wa kimataifa wa uwazi wa bajeti uliohusisha nchi 59, ikiwemo Tanzania. Utafiti huu katika Tanzania ulifanyiwa na HakiElimu na utafiti kwa jumla uliratibiwa na Mradi wa Bajeti wa Kimataifa/International Budget Project (IBP).

### Kwa Nini Utafiti Huu?

Bajeti ya taifa ni waraka mmoja wa sera ulio muhimu kabisa nchini. Unabainisha mapato ya umma, matumizi, upatikanaji wa huduma za kijamii, kama vile elimu, matunzo ya afya na maji, ubora wa maisha kwa jumla. Hivyo, upatikanaji wa taarifa ya bajeti kwa umma ni muhimu kutathmini mwitikio wa serikali kwa mahitaji ya raia na ushiriki makini wa raia katika mchakato wa bajeti. Hojaji Bayana ya Bajeti ni utafiti linganishi wa kimataifa unaotoa taswira huru isiyo ya kiserikali kuhusu uwazi wa bajeti ya serikali.

### Methodolojia

Utafiti huu ulianzishwa na Mradi wa Bajeti wa Kimataifa (IBP), wenye makao yake Washington D.C, na kuendeshwa katika nchi 59 na watafiti kutoka asasi za kiakademia au asasi zisizo za serikali katika kila nchi. Halafu, matokeo yalihakikishwa kwa ukali na wahakiki rika na wafanyakazi wa IBP.

Utafiti huu ulilenga kwenye uwazi wa bajeti katika ngazi ya Serikali Kuu tu, kimsingi ikichota taarifa kutokea kwenye taarifa ya bajeti ya 2005/06.

Utafiti ulikuwa na maswali 122 ya kuchagua yaliyobuniwa kupima uwazi wa mchakato wa bajeti duniani kote, ukitumia miongozo iliyotengenezwa na asasi za kimataifa. Utafiti huu pia ulijumlisha maswali yanayohusika na miundo ya Bunge na chombo cha nje cha ukaguzi wa mahesabu.

Nchi zilipangwa daraja kwa miitikio yao kwa maswali yanayohusiana na upatikanaji wa taarifa za bajeti. Hili liliunda msingi wa ishara ya Bajeti Bayana 2006.

Katika Tanzania, utafiti ulifanywa na Aika Kirei na Rakesh Rajani wa HakiElimu, wakisaidiwa na Geir Sundet wa REPOA/PADCO na Jacqueline Schmidt. Hatimaye, ulifanyiwa mapitio na wataalamu wa kujitegemea

### Matokeo Muhimu

Upatikanaji wa taarifa za bajeti ni changamoto muhimu kwa nyingi ya nchi zilizotafitiwa. Tanzania ilikuwa katika safu ya kati, ikiwa na alama ya 48% kwenye Ishara ya Bajeti Bayana, hivyo, kuipa nchi daraja la 25 kati ya nchi 59 zilizotafitiwa. Jedwali la 1 linaonyesha jinsi nchi mbalimbali zilizotafitiwa zilivyotenda.

**Jedwali 1: Ubora wa Taarifa ya Bajeti Inayotolewa Kwa Raia**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Taarifa Pana** | France<br>New Zealand | Slovenia<br>South Africa | U.K.<br>U.S.A. |
| **Taarifa ya Maana** | Botswana<br>Brazil<br>Czech Republic | Norway<br>Peru<br>Poland<br>Romania | South Korea<br>Sweden |
| **Baadhi ya Taarifa** | Bulgaria<br>Colombia<br>Costa Rica<br>Croatia<br>Ghana<br>Guatemala<br>India<br>Indonesia | Jordan<br>Kazakhstan<br>Kenya<br>Malawi<br>Mexico<br>Namibia<br>Pakistan<br>Papua New Guinea | Philippines<br>Russia<br>Sri Lanka<br>**Tanzania**<br>Turkey |
| **Taarifa za Kiasi** | Albania<br>Algeria<br>Argentina<br>Azerbaijan<br>Bangladesh | Cameroon<br>Ecuador<br>El Salvador<br>Georgia<br>Honduras | Nepal<br>Uganda<br>Zambia |
| **Taarifa Chache** | Angola<br>Bolivia<br>Burkina Faso<br>Chad | Egypt<br>Mongolia<br>Morocco<br>Nicaragua | Nigeria<br>Vietnam |

Katika Afrika Tanzania ilikuwa mojawapo wa watendaji wa juu. Kati ya nchi 17 za Kiafrika zilizotafitiwa, Tanzania ilifungana nafasi ya 4 na Kenya, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 2.

Baadhi ya misisitizo kutoka kwenye utafiti huo inawasilishwa hapa chini.

***Upatikanaji:*** Tanzania inatoa nyaraka 8 kati ya nyaraka 11 muhimu kwa mchakato wa bajeti na zote ziko kwenye mtandao. Hata hivyo, haitoi 'Bajeti ya Raia', Mapitio ya Ripoti ya Nusu Mwaka au Mwisho wa Mwaka. Upatikanaji ni tatizo – nyaraka, kama vile Miongozo ya Bajeti na Bajeti iliyopitishwa ni ngumu kufuatilia, zimeandikwa

| Jedwali 2: Index ya Bajeti Bayana - Africa | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Nchi** | **% ya Alama** |
| 1 | South Africa | 85 |
| 2 | Botswana | 65 |
| 3 | Namibia | 51 |
| 4* | Kenya | 48 |
| 4* | Tanzania | 48 |
| 6 | Ghana | 42 |
| 7 | Malawi | 41 |
| 8 | Zambia | 37 |
| 9 | Uganda | 31 |
| 10 | Cameroon | 29 |
| 11 | Algeria | 28 |
| 12 | Nigeria | 20 |
| 13 | Morocco | 19 |
| 14 | Egypt | 18 |
| 15 | Burkina Faso | 11 |
| 16 | Chad | 5 |
| 17 | Angola | 4 |

kwa Kiingereza tu, na ni nakala chache tu zilizochapwa.

Tovuti ya Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz) inatoa maelezo ya undani na taarifa ya wingi juu ya viwango vya kodi na ada, pamoja na mihutasari ya bajeti yenye taarifa (yaani hotuba za bajeti). Hata hivyo, haitoi toleo rahisi la bajeti au orodha ya maneno yenye taarifa katika bajeti. Haki ya kupata taarifa ya umma (Kifungu cha 18 cha Katiba ya Tanzania) hakijatungiwa sheria.

***Mambo mengine:*** Vitabu vya bajeti kuu vinatoa taarifa chache sana kuhusu shughuli za mwaka wa fedha. Kwa mfano, hakuna taarifa kuhusu matumizi ya kodi, fedha za ziada za bajeti, au matumizi ya jumla ya usalama wa taifa au usalama wa jeshi. Kuna taarifa chache sana kuhusu taarifa za uhamisho kwenda kwenye mashirika ya umma na juu ya mali za kifedha na zisizo za kifedha zilizoshikiliwa.

***Athari ya Bajeti:*** Bajeti haiakisi kwa kuonyesha malengo ya serikali yaliyotamkwa katika namna iliyo rahisi kufuatilia. Vishirio vya utendaji (maendeleo yaliyofanyika dhidi ya malengo) kwa programu za matumizi havionyeshwi katika vitabu vya bajeti.

***Ridhaa ya Bunge:*** Bunge hupokea bajeti chini ya majuma sita kabla ya kuanza kwa mwaka wa bajeti, badala ya miezi mitatu iliyopendekezwa. Pia, halina mamlaka ya kurekebisha bajeti. Ingawa Kifungu cha 99 cha Katiba ya Tanzania kinaliruhusu Bunge kupunguza matumizi au mzigo wa kodi (lakini pale tu linaporuhusiwa na utawala). Kanuni za Bunge zinalikataza Bunge kurekebisha bajeti ila tu pale linapopewa mamlaka mahususi. Zaidi ya hayo, umma na vyombo vya habari hawafikii kwa urahisi majadiliano ya Kamati ya Bunge na ripoti zao hazitolewi kwa umma.

***Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Fedha (CAG):*** CAG Hukagua matumizi yote na mara kwa mara hutoa ripoti kwa umma, ambazo hujumuisha muhutasari wa kiutendaji. Hata hivyo, hayuko huru kikamilifu kutoka Utawala – Ofisi ya CAG ni idara ya Serikali Kuu. Pia, Utawala unaweza kumwondoa CAG bila ya ridhaa ya mwisho ya mahakama au Bunge. Mwisho, inaelekea hakuna ripoti kutoka Utawala kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi wa mahesabu.

**Hitimisho na Mapendekezo**

Utafiti unaonyesha kwamba Tanzania iko katika nafasi za nusu ya juu ya nchi duniani, na ni mojawapo ya nchi zilizo wazi kabisa katika Afrika. Hata hivyo, kuna nafasi ya uboreshaji. Kuongeza ushiriki wa umma katika mchakato wa bajeti, Serikali inapaswa kushughulikia mapungufu yaliyoelezwa hapo juu. Jamii ya kiraia inaweza kusaidia kuhusu mchakato huu. Juhudi zifuatazo ni muhimu sana:

- Nyaraka zote za kabla na baada ya bajeti zipatikane kwa Kiswahili pia.
- Taarifa za bajeti zinapaswa ziweze kupatikana kwa wakati katika mtandao na maktaba za umma na ofisi za wilaya.
- 'Bajeti ya Raia,' ikiwa ni pamoja na taarifa za msingi zitolewe pamoja na bajeti au mara tu kufuatilia mapendekezo ya bajeti.
- Viashirio vya utendaji wa maendeleo yaliyofanyika dhidi ya malengo zinapaswa ziunganishwe katika bajeti.
- Bunge linapaswa kupokea bajeti walau mwezi mitatu kabla ya kuanza kwa mwaka wa bajeti. Utawala, ili kuimarisha kati zake za uwajibikaji.
- Hatua zinazochukuliwa na Utawala kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi wa mahesabu zinapaswa zitolewe taarifa hadharani kila mwaka.

*Imeandikwa na Ruth Carlitz, kutafsiriwa na Saifu Kiango, na kuhaririwa na Hebron Mwakagenda.*



SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org